**MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 21/01/2021 KATIKA UKUMBI MKUBWA WA MANISPAA**

**KU/SMC/BM/50/2021 – WALIOHUDHURIA:**

**1. WAHESHIMIWA MADIWANI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Jastin Malisawa | - | Mstahiki Meya – Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Istus Kapufi | - | Naibu Meya |
| 3. | Mhe. Dimela Kafwa | - | Diwani viti maalum |
| 4. | Mhe. Juma Mnanka | - | Diwani Kata ya Msua |
| 5. | Mhe. Adorfina Konongo | - | Diwani Kata ya Lwiche |
| 6. | Mhe. Frank Lupimo | - | Diwani Kata ya Milanzi |
| 7. | Mhe. Francis Manyika | - | Diwani Kata ya Majengo |
| 8. | Mhe. Mary Kipalasha | - | Diwani Kata ya Malangali |
| 9. | Mhe. Hadija Maufi | - | Diwani Viti Maalum |
| 10. | Mhe. Edwin Misasi | - | Diwani Kata ya Katandala |
| 11. | Mhe. Roswita Chekwe | - | Diwani Viti Maalum |
| 12. | Mhe. Janeth Sinyangwe | - | Diwani Viti Maalum |
| 13. | Mhe. Colnel Kafumu | - | Diwani Kata ya Sumbawanga |
| 14. | Mhe. Anthony Kayombo | - | Diwani Kata ya Chanji |
| 15. | Mhe. Gabriel Kimamala | - | Diwani Kata ya Izia |
| 16. | Mhe. Charles Chakupewa | - | Diwani Kata Ya momoka |
| 17. | Mhe. Andrea Cheka | - | Diwani Kata ya Kizwite |
| 18. | Mhe. Juma Dawood Nzegere | - | Diwani Kata Mazwi |
| 19. | Mhe. Agustino Ngoani | - | Diwani Kata yaPito |
| 20. | Mhe. Syriacus Pangani | - | Diwani Kata ya kasensne |
| 21. | Mhe. Cadius Mtullo | - | Diwani Kata ya Ntendo |
| 22. | Mhe. Leticia Kipeta | - | Diwani Viti Maalum |
| 23. | Mhe. Sangu Maarifa | - | Diwani Kata Mollo0 |
| 24. | Mhe. Anna Mwamba | - | Diwani Viti Maalum |
| 25. | Mhe. Lameck Pondamali | - | Diwani Kata ya Mafulala |

**A. WATAALAM**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Jacob J. Mtalitinya | - | Mkurugenzi wa Manispaa Katibu |
| 2. | Ndg. Goodluck Magova | - | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii |
| 3. | Ndg. Andrew Zumba | - | Afisa Uchaguzi |
| 4. | Ndg. Eliud Fungo | - | Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika |
| 5. | Ndg. Ardius Kwimba | - | Kaimu Mchumi Manispaa |
| 6. | Ndg. Joseph Nkonjera | - | Afisa Misitu |
| 7. | Ndg. Lucy Mwakyusa | - | Kaimu Afisa Utumishi na Utawala |
| 8. | Ndg. Thadeo Maganga | - | Afisa Maliasili na Utalii |

9. Ndg. George Nyanga - Afisa Usafirishaji
10. Ndg. Deogratius Masalu - Kaimu Mkaguzi wa Ndani
11. Ndg. Peter Tarimo - Afisa Elimu Msingi
12. Ndg. Mussa Nginila - Afisa Manunuzi
13. Ndg. Fortunatus C. Lyapa - TSC
14. Eng. Denis Eliakimu - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi
15. Ndg. Jenifrida Manuma - Afisa TEHAMA
16. Ndg. Mathew Madama - Mwanasheria Manispaa
17. Ndg. Salustian Shirima - Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika
18. Ndg. Oswald Temba - Afisa Afya
19. Dr. Witness Mbwelwa - Kaimu Mganga Mkuu
20. Ndg. James Makwinya - Mwananssheria Manispaa
21. Ndg. Shupai Mwazembe - Kaimu Afisa Biashara Manispaa
22. Ndg. James Kajungu - Kaimu Afisa Mipango Miji
23. Ndg. Salustian Shirima - Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika
24. Ndg. Muyemba - Kaimu Afisa Mazingira

**C: WAALIKWA**

1. Ndg. Sebastian Waryuba - Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga
2. Ndg. Neema Fungo - Jeshi la Akiba
3. Ndg. Sabina Mwajeka - Afisa Tarafa Itwelele
4. Ndg. Dafroza Msechu - Afisa Tarafa Lwiche
5. Ndg. Mohamed Mlumba - UHAMIAJI
6. Ndg. J. Mollel - Afisa Usalama Wilaya
7. SSP Maria D. Kway - Mkuu wa Polisi Wilaya
8. Ndg. Christina Mzena - DAS
9. Ndg. Melkior Komba - Magereza
10. Ndg. Tabu Shaaban - Katibu CCM Wilaya
11. Ndg. Chami Chasuka - Mwenyekiti CCM
12. Ndg. Elizabeth Simkway - Afisa Serikali za Mitaa
13. Ndg. Ndg. James Mbungano - TAKUKURU
14. Ndg. Baraka Lusajo - ITV
15. Ndg. Sammy Kisika - AZAM TV
16. Ndg. Edith Peter - VOS
17. Ndg. Misri Mwasenga - STAR TV
18. Ndg. Peter Helatano - Global TV
19. Ndg. Musa Mwangoka - Mwananchi

20. Eng. Samson Kelesi - TARURA
21. Eng emmenuel Kudema - TARURA

**25. SEKRETARIETI**

1. Ndg. Khadija Dalasia - Katibu wa Vikao

**KU/SMC/BM/51/2021 – KUFUNGUA KIKAO:**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao, Mwenyekiti alianza kwa kusoma dua. Mwenyekiti alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuweza kutufikisha siku ya leo ambapo alisema kuwa kikao cha leo ni muendelezo wa vikao vya bajeti kwa mujibu wa sheria zetu . Pia alitumia fursa hii kumpongeza mhe Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kutupatia fedha kwa ajili ya miradi mbalimali ikiwemo ujenzi wa Madarasa ya UVIKO na ya Tozo, Mabweni , Maabara na Viftuo vya Afya.
Aliwaambia wajumbe kuwa ili bajeti iweze kukamilika na kuanza kutumika ni lazima ipitishwe na Bunge. Mwenyekiti Alifungua kikao mnamo saa 4.17 Asubuhi

**KU/SMC/BM/52/2021 – KUTHIBITISHA DONDOO:**
Ziliwasilishwa dondoo za kikao cha tarehe 31.08.2021 wajumbe kwa kauli moja walizipokea na kuzithibitisha.

**KU/SMC/BM/53/2021 – MAPENDEKEZO NA MPANGO WA BAJETI WA TARURA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**
Meneja wa TARURA aliwasilisha Mapendekezo na Mpango wa bajetu ya TARURA kwa Mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha Tsh 2,271,910,000.00 zinategemewa kutumika katika matengenezo ya Barabara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kama ifuatavyo:

**A. Mfuko wa barabara (Road Fund)**
Tunategemea kupokea kiasi cha **Tshs.** 1,271,910,000.00 ambacho kitatumika kufanya matengenezo yafuatayo:

(i) Matengenezo ya kawaida urefu 68.48km Tshs. 280,500,000.00

(ii) Matengenezo katika maeneo korofi urefu 20.79km – Tshs. 250,000,000.00

(iii) Matengenezo ya muda maalum urefu 7.55km – Tshs. 386,000,000.00

(iv) Ujenzi wa Madaraja na Mifereji – Tshs. 286,000,000.00

(v) Gharama za ufuatiliaji na usimamizi – Tshs. 88,410,000.00

**B. Mfuko wa Tozo:**

Tunategemea kupokea kiasi cha Tshs. 500,000,000.00 kufanya matengenezo yafuatayo:-

(i) Kufungua barabara mpya kiasi cha Tshs . 260,000,000.00

(ii) Matengenezo kiwango cha changarawe Tshs. 240,000,000.00

**C. Mfuko wa Jimbo:**

Tunategemea kupokea kiasi cha Tshs. 500,000,000.00 kufanya matengenezo ya barabara katika kiwango cha lami.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kusahuri kama ifuatavyo;

**Ushauri**

- Waheshimiwa Madiwani waliomba pindi TARURA wanapofanya kazi ya Kufungua barabra au mitaa pbasi washirikishwe ili waweze kuwaonesha barabra amabazo zina umuhimu ambazo zinatakiwa kufunguliwa kwani wao ndio wanapokea maoni ya wananchi.
- Waheshimiwa Madiwani waliomba TARURA iangalie sana Vivuko vya kuunganisha kijiji na kijiji Mtaa na Mta kata Na kata kwabni vivuko vingi havipitiki na ndio njia zinazotumika na wananchi. Vivuko Ambavyo waliomba vifanyiwe kazi ni ;
    - Kivuko cha Mtaa wa Kaloleni na Kamambangasa kwa Kata ya Majengo
    - Vivuko kati Kata ya Lwiche
    - Kivuko kati ya Mtaa wa Senti na Malangali
    - Kivuko kati ya Kantalamba na Shule ya Mwenge
- Waheshimiwa madiwani waliomba kuwa Bajeti au Mapendekzo ya Bajeti ya TARURA yaanzie kwenye WDC kwa Kata kuwasilisha mapendekezo yao kuona ni Barabara zipi zinanze kushughulikiwa kwani wao ndio wenye Kata na wanajua maeneo korofi zaidi

**AZIMIO**

- TARURA wafanye tathimini ya kina ili waweze kujua na kutambua ni barabara zipi hazipo kwenye Mtandao wa Tarura ili fedha ziweze kutafutwa au kuwashirikisha wananchi kuzifungua barabra hizo.
- Mchakato w Bajeti ya TARURA, RUWASa uanzie kwenye Kata
- Halmashari na TARURA waweke Bajeti ya kusafisha mitarao katika bajeti ya Mwaka 2022/2023.

- TARURA wawasilishe Ombi la kutengeneza barabra ya Mzunguko (By Pass Road) ya Kutoka Katumba – Milanzi yenye urefu wa km 20 kwa kiwango cha Lami ili kupunguza Msongamano wa malori hapa mjini.
  7

Baraza la Madiwani liliridhia na kupitisha Mapendekezo hayo ya Mpango wa bajeti ya TARURA wa Tsh 2,271,910,000.00

**KU/SMC/BM/51/2021 – KUFUNGA KIKAO:**
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao aliwwashukuru wajumbe kwa michango yao mizuri ambayo ina nia ya kuiletea maendeleo Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Mwenyekiti aliwashukuru kwa kusema wajumbe wameshiriki kikamilifu kwa kuwa wawazi na kuchangia mengi yenye tija. Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 5.40 Asubuhi

Umesambazwa na ……………………. Saini ……………………. Tarehe ………………

**UMETHIBITISHWA / HAUKUTHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| …………………………... | …………………………….. |
| Jacob J. Mtalitinya | Mhe. Jastin Malisawa |
| **Mkurugenzi Manispaa** | **Mstahiki Meya** |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 31/08/2021 KATIKA UKUMBI MKUBWA WA MANISPAA**

| NA | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1 | **AZIMIO**<br>Hoja Binafsi ya Mhe. Juma Mnaka ikajadiliwe katika Kamati ya Uchumi Afya na Elimu kulingana na kanuzi za kudumu zinavyoelekeza | **KATIBU** | Hoja Binasfi ya Mhe. Juma Mnanka iliwasilishwa ktaika Kikao cha Kamati ya Uchumi Afya na Elimu kilichoketi tarehe 27.11.2021 na Kikao kiliazimia kuwa Maeneo yote ya Mji hayaruhusiwi kulima mazao marefu kama vile Alizeti, Mahindi, Mtama, Ngano kwa mujibu wa Kanunzi zilizopo |